






# Michezo ya Fungu za Kumbukumbu








Kristina Krauss

# Michezo ya Fungu za Kumbukumbu

Kila wakati...
... ni vizuri kuwasaidia wanafunzi wako kukariri fungu za Biblia. Bila kujali ni mtaala gani unaotumia, kila timu itakuwa na fungu muhimu kwa kila somo. Nafurahia kuwasilisha michezo ya fungu za kumbukumbu ambayo itasaidia
unapofundisha watoto Biblia. Haitasaidia tu wanafunzi kurudia maandiko, lakini pia itasaidia kukumbuka, hivyo watakumbuka Biblia wakati wanapohitaji kuitumia kwa maisha yao ya kila siku.

Nimekuwa kanisani maisha yangu yote na nakumbuka nikiwa mtoto, walimu wangu walinisaidia kukumbuka mistari ya Biblia na kunizawadi kila wakati nilifanya hivyo. Nilipata stika, pipi na hata Biblia yangu ya kwanza kwa kuhudhuria darasa, kukumbuka mistari, na kwa kila njia ambayo nilishiriki. Sijui ikiwa ni wazo nzuri kutoa tuzo nyingi, lakini nakumbuka vizuri kwamba zaidi ya yote niliyoweza kushinda nilipata kushinda nafasi ya kwenda kwenye kambi ya Kikristo ya msimu wa joto. Niamini ndugu na dada, nilitia bidii ili niweze kwenda, na niliweza kwenda kambi kwa miaka 5 mfululizo bila malipo yoyote; na sababu nilijua tu
kukumbuka mafungu!
Nawashukuru ndugu na dada ambao waliwekeza katika maisha yangu. Sasa nina huduma inayoleta madadiliko kwa maelfu ya watoto, na bado ninaweza kukumbuka mistari niliyojifunza nikiwa mtoto. Nataka kukuhimiza kwamba kazi yako sio ya bure. Hakuna njia yoyote ya kugundua wanafunzi wako walio darasani lako watakuwa nini baadaye! Wanaweza kuwa mchungaji, daktari au rais! Je, baadaye watahitajije mafungui unaowafundisha wiki hii?

Na ili kukusaidia kujifunza michezo ya fungu za kumbukumbu, ningependa kukuelezea kuhusu watoto hawa wanne wafuatao, ambao wako tayari kutoa msaada kwa mradi huu. :) Charles, Blessie, Samuel, Araceli




Baraka juu ya kazi yako muhimu!
Dada Kristina Krauss





1. Kupitisha kwa kupokezana
Watoto wanaketi karibu na meza. Mtu mmoja anaandika neno la kwanza au mstari wa kifungu (au kumbukumbu) kwenye karatasi na kupitisha kwa mtu wa pili ambaye anaandika neno linalofuata au

msitari, na kadhalika hadi fungu litakapomalizika. Na mtoto anayefuata anaanza fungu lingine, na kadhalika.Kwa kupima muda unaotumiwa na watoto na kuona ikiwa "watamaliza" kabla ya muda wa zamu iliyopita, unaweza kuongeza ladha katika shughuli hiyo .Kupima muda wa shughuli kutakuwezesha kuamua ni mafungu yapi na gani utakayojumuisha (kwa mfano, angalia ni mafungu mangapi wanaweza kuandika chini ya dakika 10).



2. Mbio za Kupokezana
Gawanya watoto katika timu mbili. Weka ubao, bodi nyeupe, au karatasi kubwa kwa umbali fulani kutoka eneo la kuanza. Patia mtoto wa kwanza wa kila timu kifaa cha kuandika na kusema kwa sauti "Enda" na kumfanya akimbie kwenye ubao na kuandika neno la kwanza la mstari.Kisha kumfanya arudi kwenye kwenye timu yake na kumpokeza mwenzake wa pili kifaa cha kuandika.Timu ya kwanza kufanikiwa kuandika fungu inashinda.

3. Kupokezana Mrija
Kata mirija ya kunywa katika nusu (takriban vipande 4), moja kwa kila mtoto.(Mirija mipana ni bora zaidi.)Andika kila neno la fungu kwenye kipande tofauti cha karatasi, na kutengeneza fungu kwa kila timu.Gawanya darasa katika timu. Weka maneno kwenye meza kwa kila timu. Kama mbio ya kupokezana, kila mwanatimu lazima atachukua neno moja la fungu akitumia mrija wake na kubeba hadi kwenye meza ya timu yao iliyo upande wa pili wa chumba.Timu ya kwanza ya kutengeneza na kusoma fungu kwa sauti ndio washindi.





4. Futa Neno
Andika fungu ya kumbukumbu kwenye bodi. Futa neno moja kutoka kwa msitari kwa wakati mmoja, kila wakati unawauliza watoto kukariri fungu.

5. Vipande vya karatasi
Andika kila neno la fungu la kumbukumbu juu ya kipande cha karatasi. Watoto wanapaswa kupanga vipande kwa usahihi. Unaweza pia kushikiza kipande cha karatasi ukitumia utepe katika upande wa mbele wa kila mtoto na kuwafanya wasimame kwa utaratibu sahihi.



6. Uliza Maswali
Mchezo huu ni sawa na uliopita ambapo uliweka kila neno la fungu katika kipande tofauti cha karatasi, ila tu wakati huu shikiza kipande katika upande wa nyuma wa kila mtoto ukitumia utepe. Wafanye waulize wengine maswali ili kugundua neno lililo nyuma yao, na kisha wapange laini kwa usahihi.

7. Mchezo wa Tic-tac-toe
Mchezo wa Fungu la Kumbukumbu wa Tic-Tac-toe ni rahisi sana kucheza na hauhitaji matayarisho ya mapema .Ili kucheza, weka safu 3 za viti 3 katikati ya darasa na kuvitumia kama bodi yako ya Tic-Tac-Toe. Ikiwa hutumii viti katika darasa lako, unaweza kutumia sahani za karatasi au karatasi kwenye sakafu na kutumia kama bodi yako ya Tic-Tac-Toe. Huku kila mwanatimu akikariri mstari wao wa kumbukumbu kwa usahihi, wanafaa kuchagua nafasi kwenye bodi ya Tic-Tac-Toe na kukaa au kusimama pale. Timu ya kwanza kufanikiwa kupata Tic-Tac-Toe wanashinda.





8. Herufi moja kwa wakati
Andika herufi ya kwanza ya kila neno la fungu la kumbukumbu kwenye bodi. Kisha watoto wanaandika fungu.

9. Kiazi Moto
Tumia mfuko wowote kama "kiazi moto" na kuweka ndani vipande vya karatasi vilivyo na neno moja la mstari wa kumbukumbu. Watoto wote wanaketi kwa mduara mmoja mkubwa, kisha anzisha muziki. Muziki unakaposimama, mtoto anachukua kipande kimoja cha karatasi kutoka kwenye mfuko wa karatasi. Wanaweza kuweka kwenye bodi wakitumia utepe au kuweka kwenye sakafu katikati ya mduara. Himiza watoto kusaidiana ili kuweka fungu la kumbukumbu katika utaratibu sahihi.





10. Karatasi ya Mpira wa kikapu
Andika kila neno la fungu lako la kukumbuka kwenye kipande cha karatasi na kukunja kama mpira mdogo wa kikapu. Gawanya darasa lako katika timu mbili na utengeneze "mipira ya kikapu" ya kutosha ya fungu la kumbukumbu. Weka pete ndogo ya mpira wa kikapu sehemu ya mbele ya darasa. Ikiwa hutapata pete ya mpira wa kikapu, unaweza pia kutumia kikapu cha taka au aina nyingine ya kikapu. Fanya watoto wachukua zamu wakifanya "kapu". Wanapofanya kapu, timu inafungua mpira wa kikapu ili kugundua neno kutoka kwenye mstari wa kumbukumbu.Timu ya kwanza kukamilisha fungu la kumbukumbu na kupanga kwa utaratibu sahihi ndio washindi.

11. Waza
Fanya watoto waandike fungu hilo, na kuchora picha nyingi iwezekanavyo kuhusu maneno yake.





12. Ping Pong
Mtoto anasema kwa sauti mstari wa kwanza wa fungu, kisha mwingine anasema mstari wa pili wa fungu, na kadhalika. Hii inaweza kuchezwa kwa jozi au katika timu huku watoto wakiangaliana katika laini.

13. Imba 'Rap'
Tafuta au tengeneza muziki na kuandika fungu mahala ambapo wanafunzi wanaweza kuona. Fanya wanafunzi waweze 'kurap' kwenye muziki kwa kutumia maneno kutoka kwenye fungu. Unaweza kuanza kama kikundi, wavulana pekee, wasichana pekee, na hatimaye ruhusu mwanafunzi mmoja kwa wakati mmoja ikiwa wanataka. Watoto wataipenda!





14. Mlipuko wa puto
Weka hewa kwenye puto, puto moja kwa kila neno la fungu la kumbukumbu. Kwa alama ya kudumu, andika neno moja la fungu la kumbukumbu juu ya kila puto. Tumia utepe wazi wa kufungia, weka puto katika ukuta kwa mpangilio sahihi (ikiwa kuna muda wa kutosha, watoto wanaweza kuchukua zamu na kufanya hili). Ikiwa unaweka puto wakati darasa linaendelea, uliza darasa lote

kusoma kile kinachowekwa. Baada ya kuweka puto zote, kuwa na wanafunzi wa kujitolea kwenda na kulipua puto yoyote (kutumia "pini ya kudunga" inafanya kazi vizuri), ikifuatiwa na kila mtu akisema fungu kwa pamoja wakati kila puto inalipuliwa.

15. Mafumbo ya Kupanga Vipande



Fanya kila mtoto aandike fungui juu ya kipande cha karatasi ya rangi, chora mistari ya mafumbu na kukatakata katika vipande.(Ikiwa huna muda wa kutosha, tayarisha mafumbo mapema.) Kuwa na mashindano ya kupanga mafumbo pamoja. Mshindi ni mwanafunzi au timu ya kwanza kusimama na kusoma fungu kwa sauti baada ya kumaliza mafumbo yao.



16. Mchezo wa Mpira wa Muziki

Kwanza, jifunze fungu, rudia mara kadhaa, au kwa mchezo wowote. Kisha aanzisha muziki na kufanya watoto wapitishe mpira kwenye mduara au darasani (sheria nzuri unaweza kutumia ni, "hakuna kurusha mpira"). Muziki unaposimama, mtoto aliye na mpira anapata kusema fungu au anachagua mtu atakayesema fungu hilo kwa ajili yake. Endelea mpaka wote wawe na fursa ya kusema fungu hilo wenyewe.

17. Kurusha Mfuko wa Maharage



Fanya watoto waketi katika mduara kwenye sakafu. Andika fungu kwenye bodi, au kwenye kipande cha karatasi ambacho watoto wanaweza kukiona. Kisha fanya watoto wapitishe mfuko wa maharagwe (au karatasi iliyokunjwa, au mfano wa mnyama, nk) kwa mtoto aliye kando yao, yeyote anayeshika mfuko wa maharagwe anasema neno linalofuata la fungu hilo. Ili kufanya mambo magumu zaidi, ruhusu wanafunzi kurusha mfuko wa maharagwe kwa yeyote katika mduara ili kusema neno linalofuata la fungu.



18. Mchezo wa Kuruka

Tumia utepe wa kufunika kutengeneza eneo la mchezo wa kuruka katika sakafu. Andika maneno ya fungu la kumbukumbu kwenye karatasi na kufunga kwa utepe juu ya mraba wa mchezo (weka utepe vizuri kwenye karatasi ili watoto wasiangushwe na maneno). Fanya darasa kupanga laini katika kila upande wa eneo la mchezo ili waweze kuona maneno wakati watoto wanachukua zamu za kuruka. Mtoto anaporuka katika kila mraba, darasa linasoma fungu na kuendelea.

19. Kinyang'anyiro cha alfabeti




Gawanya darasa katika makundi mawili au matatu na kutoa kikombe cha alfabeti ya nafaka au pasta kwa kila kikundi. Fanya watoto kutumia herufi kutengeneza maneno kutoka kwenye fungu la kumbukumbu. Kikundi kinachotengeneza maneno mengi ndio washindi.




20. Kuigiza

Tumia ishara za mwili kueleza fungu la kumbukumbu. Mchezo huu ni mzuri kwa sababu unatumia kuona, kufanya, na kusikiza.

21. Viti vya muziki
Panga kiti kwa kila mtoto na uziweke kwenye mduara. Kata vipande mbalimbali vya karatasi za rangi na kuziweka upande wa nyuma wa viti ukitumia utepe.Kila rangi inapaswa kuwekwa kwa angalau viti vitatu. Anza muziki na kufanya watoto kutembea karibu na viti. Muziki unaposimama, watoto wanaketi kwa haraka. Kisha mwalimu anataja rangi, na kila mtoto ambaye ameketi katika kiti ambacho rangi hiyo imewekwa anasimama na kusema fungu la kumbukumbu. Ikiwa mwalimu anasema nyekundu, kila mttoto aliye kwenye kiti kilicho na karatasi nyekundu anasimama na kusema fungu kwa pamoja.





22. Kisia ni Nani
Chagua mtu wa kujitolea ambaye anafaa kwenda na kusimama kando na mwalimu huku akionyesha mgongo wake na fungu la kumbukumbu likionekana. Yeyote anayefundisha fungu hilo anaonesha neno katika fungu na kuagiza kikundi kusoma fungu lakini wanapiga * makofi* ikifika katika neno lililochaguliwa. Kisha mtoto aliyejitolea akisia ni neno gani linakosa.

23. Mlima wa Mwangwi
Gawanya kikundi katika timu tatu, kwa mfano; walimu, wavulana, na wasichana.Timu moja inaanza kwa kusema neno la kwanza au msitari wa fungu la kumbukumbu, timu ya pili inarudia, na kisha timu ya mwisho. Endelea na mchezo, na kuongeza ladha kwa kubadilisha jinsi unavyosema kila neno. Vidokezo ni kama: kusema kwa sauti ya chini, kwa sauti ya juu, kwa haraka, kwa sauti ya mngurumo, kama nyangumi akitafuta Nemo, kwa haraka zaidi, pole pole zaidi, opera, kwa utulivu kama panya, chini ya maji, au kama roboti.  Furahia hilo!






24. Nukuu ikiwa...
Nukuu fungu ikiwa wewe... ulikula kiamsha kinywa asubuhi hii, ulioga usiku uliopita, una macho ya rangu ya hudhurungi, unapenda brokoli, ulitengeneza kitanda chako asubuhi, una dada, umevaa nguo nyekundu, nk. Hii ni njia rahisi ya kurudia fungu mara nyingi ili kuwasaidia watoto kuikumbuka.

ZIADA ZIADA ZIADA ZIADA ZIADA

Nyuki inayotahajia
Baada ya wanafunzi wako kumaliza kitengo cha madarasa, kagua mafungu yote na "nyuki ya kutahajia". Panga kila fungu sehemu ya mbele na kuwa na mtoto mmoja kwa wakati mmoja. Anza fungu kwa maneno machache ya kwanza, kisha ona ikiwa wanaweza kumalizia fungu. Ikiwa hawawezi wanafaa kukaa chini, na mtoto anayefuatia anajaribu kumalizia fungu. Endelea mpaka ni mtoto mmoja tu anayebaki kama amesimama na ambaye ndiye mshindi. (Hakikisha umekagua mafungu yote ili kuchangia katika "nyuki ya kutahajia" ili kufarahisha zaidi.)

Fungu la Kumbukumbu Napenda Zaidi:

- "Je, si mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na shujaa. Usihofu wala usivunjike moyo, kwa kuwa BWANA Mungu wako atakuwa pamoja nawe kokote uendako." Yoshua 1:9
- "Lakini mimi na nyumba yangu, tutamtumikia Bwana."Yoshua 24:15b
- Nayainua macho yangu nitazame vilima, msaada wangu utatoka wapi? Msaada wangu hutoka kwa BWANA, Muumba wa mbingu na dunia. Zaburi 121:1-2
- Tazama jinsi miguu ya wale waletao habari njema ilivyo mizuri juu ya milima, wale wanaotangaza amani,wanaoleta habari njema, wanaotangaza wokovu, wauambiao Sayuni,"Mungu wako anatawala!" Isaya 52:7
- Ombeni nanyi mtapewa; tafuteni nanyi mtapata; bisheni nanyi mtafunguliwa mlango. Mathayo 7:7
- Ndipo akawaambia wanafunzi wake, "Mavuno ni mengi lakini watendakazi ni wachache. Kwa hiyo mwombeni Bwana wa mavuno, ili apeleke watendakazi katika shamba lake la mavuno."Mathayo 9:37-38
- Bwana wake akamwambia, 'Umefanya vizuri sana, mtumishi mwema na mwaminifu! Umekuwa mwaminifu kwa vitu vichache; nami nitakuweka kuwa msimamizi wa vitu vingi. Njoo ushiriki katika furaha ya bwana wako!' Mathayo 25:21
- "Ninawaambia kwamba yeyote atakayenikiri mbele ya watu, Mwana wa Adamu naye atamkiri mbele za malaika wa Mungu. Luka 12:8
- "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Yohana 3:16
- Lakini mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, Uyahudi kote na Samaria, hadi miisho ya dunia." Matendo 1:8
- Tubuni basi mkamgeukie Mungu, dhambi zenu zifutwe, ili zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwepo kwake Bwana. Matendo 3:19
- kwa kuwa wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Warumi 3:23
- Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu. Warumi 6:23
- Kwa hiyo, ndugu zangu, nawasihi kwa rehema zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu na inayompendeza Mungu, hii ndiyo ibada yenu yenye maana. Msifuatishe tena

mfano wa ulimwengu huu, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu. Ndipo mtaweza kuonja na kuhakikisha ni nini mapenzi ya Mungu yaliyo mema, yanayopendeza machoni pake na ukamilifu. Warumi 12:1-2

- Lakini aliniambia, "Neema yangu inakutosha, kwa kuwa uweza wangu hukamilika katika udhaifu." 2 Wakorintho 12:9

- Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, wala si kwa matendo yenu mema. Hii ni zawadi kutoka kwa Mungu, si kwa matendo, ili mtu yeyote asije akajisifu. Waefeso 2:8-9

- Kwa maana sisi ni kazi ya mikono ya Mungu, tulioumbwa katika Kristo Yesu, ili tupate kutenda matendo mema, ambayo Mungu alitangulia kuyaandaa tupate kuishi katika hayo. Waefeso 2:10

- Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake. Vaeni silaha zote za Mungu ili kwamba mweze kuzipinga hila za ibilisi. Kwa maana kushindana kwetu si juu ya nyama na damu, bali dhidi ya falme, mamlaka, dhidi ya wakuu wa giza na majeshi ya pepo wabaya katikaulimwengu wa roho. Waefeso 6:10-12

- Msijisumbue kwa jambo lolote, bali katika kila jambo kwa kuomba na kusihi pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Nayo amani ya Mungu, inayopita fahamu zote, itailinda mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu. Wafilipi 4:6-7

- Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, na udhahiri wa mambo yasiyoonekana. Waebrania 11:1

- Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu, kwa maana yeyote anayemjia Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko na ya kuwa huwapa thawabu wale wamtafutao kwa bidii. Waebrania 11:6

- Kwa sababu hii, kwa kuwa tumezungukwa na wingu kubwa namna hii la mashahidi, basi na tuweke kando kila kitu kinachotuzuia na ile dhambi inayotuzinga kwa urahisi, nasi tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa kwa ajili yetu. na tumtazame sana Yesu mwanzilishi na mkamilishaji wa imani yetu, yeye ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake alistahimili msalaba, bila kujali aibu ya huo msalaba, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu. Waebrania 12:1-2

- Ndugu zangu, hesabuni kuwa ni furaha tupu mnapopatwa na majaribu mbalimbali, sababu mnajua ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi timilifu, ili mpate kuwa wakamilifu, mmekamilishwa, bila kupungukiwa na kitu chochote. Yakobo 1:2-4

- Basi kuweni watendaji wa Neno wala msiwe wasikiaji tu, huku mkijidanganya nafsi zenu. Yakobo 1:22

- Vivyo hivyo, ninyi mlio vijana watiini wazee. Nanyi nyote imewapasa kujivika unyenyekevu kila mtu kwa mwenzake, kwa kuwa,"Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema." 1 Petro 5:5

- Kama tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki, atatusamehe dhambi zetu na kutusafisha kutoka kwenye udhalimu wote. 1 Yohana 1:9

- Kwa namna hii twaweza kulijua pendo la Mungu: Kwa sababu Yesu Kristo aliutoa uhai wake kwa ajili yetu. Nasi imetupasa kuutoa uhai kwa ajili ya hao ndugu. 1 Yohana 3:16

- Wapendwa, tupendane, kwa kuwa pendo latoka kwa Mungu. Kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu. Yeye asiyependa hamjui Mungu, kwa sababu Mungu ni pendo. 1 Yohana 4:7-8

- Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo na kwa neno la ushuhuda wao. Wala wao hawakuyapenda maisha yao hata kufa. Ufunuo 12:11

- Tazama, naja upesi! Thawabu yangu i mkononi mwangu, nami nitampa kila mtu sawasawa na alivyotenda. Ufunuo 22:12

Sura ya Kumbukumbu Napenda Zaidi:

Zaburi 1; Zaburi 15; Zaburi 23; Zaburi 27; Isaya 61; Mathayo sura 5-7; Warumi 12; 1 Wakorintho 13; Yakobo 1-5.